

## MATUNZO

Kubadilisha yenyi kukosa ; kufanya tena matuta ao billon yenyi iliharibika na mvua wala mapitio za nyama ; wakati wote kupalia majani mabaya yanayoota.

## Mavuno

Wakati wa kuvuna inafatana na kukomaa kwa kila namna na inabandilika tokea miezi 3 kwa miezi 5. Mavuno yanaweza kufanyika kadiri ya mahitaji tokea miezi 3 kwa miezi 4. Ikiwa mavuno yanachelewa kupita miezi 6, huweza kupata viazi vyinyi kuanza kuoza.

Ni ya lazima mavuno yafanyike kwa mwezi ine baada ya kupada viazi , ikiwa imetayarishwa kwa soko.

## KUCHUNGA

Viazi isipotunwza vizuri baada ya kuvunwa vinaweza kuoza. Kwa hivi, ni vema kuchagua viazi isiyokatwa au isiyoodolewa ngozi kwa kuvichunga muda murefu. Viazi vinawekwa vizuri pahali kavu na kwenyi hewa. Viazi vyinyi kukaushiwa juani vianaweza kuchugwa muda wa juma mengi.



Programme de Relance de la Recherche Agricole et Forestière  
en République Démocratique du Congo

Projet 9 ACP ZR 13/1 (GCP/DRC/036/EC selon codification FAO)

Financé par l'Union européenne et exécuté par la FAO

Ce document a été réalisé avec l'aide financière de l'Union européenne.  
Les opinions exprimées dans le présent document ne reflètent pas nécessairement l'opinion officielle de l'Union européenne.

## Ufundi wa mlimo ya viazi sukari



**INERA**  
13, Avenue des Cliniques, Kinshasa/Gombe  
B.P. 2037, Tél. 098185431- 09935175  
E-mail : [inera\\_dg@yahoo.fr](mailto:inera_dg@yahoo.fr)  
Site Internet : [www.inera-rdc.org](http://www.inera-rdc.org)

## Tangulizi

Viazi sukari (patate douce) inalim-wa zaidi kwa malisho ya mtu. Lakini inawezekana pia kiitumia kwa kulisha nyama. Inafunika vizuri udongo pamoja na majani yake mengi na vibua vyake virefu ; inasaidia basi kwa kukinga udongo ili mvua isiubebe kwa maporomo-ko.

Majani ya kiazi cha sukari yapo maboga mazuri sana. Namna ya kiazi cha sukari chenyi rangi ya majano (chair orange) yako tajiri kwa vitamine A.

### Matayarisho ya shamba

Kulima na kugeuza sana udongo ni lazima sana kama shamba ipo yenyi kunyoroka. Lakini, kwa kupata mavuno mengi, ni vema kulima juu ya billon ao matuta. Urefu wa billon unatafauti ; billon ya 3 kwa 6 metri yapo mazuri na yafanyiziwa kwepesi.

### Matayarisho ya matambazi za kupanda

Matambazi ya kupandwa inavunwa kwa shamba inyotimiza ya umri wa miezi 5. Sehemu inayokatwa ni ya mwisho ya matambazi, yaani sehemu ya ujana.inayoitwa “bouture apicale”, (basi ina tofauti ya na miti ya mhogo kwenye wanakamata sehemu yenyi imekoma sana)

Matambazi inapashwa kuwa 30-40 sentimetri ya urefu . Ni vema inapandwe mbio baada ya kukatwa. Inawezekana vile vile kuwekwa ikiwa shamba haijakuwa tayari kwa kupanda. Hivi inafaa kuyichunga pahali kavu na kwenyi hewa na kivuli. Majani yote yanatoshwa, bila majani ya juu. Kuyiweka ndani ya hali hii yaweza kuchunwa mpaka juma 3



Matambazi tayari kupandwa.

### Kupanda

Kupanda inaweza kufanyizwa pahali yenyi kunyoroka, ao juu ya matuta ao juu ya billon yenyi kuachana na 100 cm x 30 cm, ndiyo kusema mimea 33.000 kwa hektari moja. Hupanda mimea 3 kwa tuta ao hufanya mistari miwili ya shimo inapangwa en quinconce juu ya billon na hulima mmea moja kwa shimo. Wanapashwa kingiza  $\frac{3}{4}$  ya mmea ndani ya udongo na kuwacha tuu kichwa cha mmea yenyi majani juu ya udongo.